

## بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

### 1. RAMADHANI NI MWEZI WA BARAKA KWA KAULI YA MTUME Swala na salamu zimfikie:

« أَتَاكُمْ رَمَضَانُ شَهْرٌ مُّبَارَكٌ »

“Umekujieni (mwezi wa) Ramadhani mwezi wenye baraka<sup>1</sup>”.

### 2. HAIFAI KUFUNGA KWA KUITANGULIA RAMADHANI:

« لَا تَقْدَمُوا رَمَضَانَ بِصَوْمِ يَوْمٍ وَلَا يَوْمَيْنِ إِلَّا رَجُلٌ كَانَ يَصُومُ صَوْمَهُ، فَلْيَصُمْ ذَلِكَ الْيَوْمَ »

“Asiitangulie mmoja wenu Ramadhani kwa kufunga siku moja au mbili (kabla yake) isipokuwa mtu ambaye alikuwa anafunga fungu yake (ya kawaida), basi na afunge siku hiyo (hakuna vibaya)<sup>2</sup>”.

### 3. HAIFAI (NI HARAMU) KUFUNGA SIKU YA SHAKA:

« مَنْ صَامَ الْيَوْمَ الَّذِي يُشَكُّ فِيهِ فَقَدْ عَصَى أَبَا الْقَاسِمِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ »

“Atakaefunga siku ambayo hutiliwa shaka ndani yake basi amemuasi Abul Qassim (Mtume) swala na salamu zimfikie<sup>3</sup>”.

### 4. FUNGA YA RAMADHANI NI MOJA YA NGUZO TANO ZA KIISLAMU:

« بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ شَهَادَةِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ وَالْحَجِّ وَصَوْمِ رَمَضَانَ »

<sup>1</sup>- Sunan Nasaai (2106).

<sup>2</sup>- Bukhari (1914) na Muslim (1082).

<sup>3</sup>- Sunan Nasaai (2188)

“Umejengwa uislamu juu ya nguzo tano: Kushuhudia kwamba hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki ila Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wake, Kusimamisha swala, Kutoa zaka, Kuhiji na Kufunga (mwezi wa Ramadhani)<sup>4</sup>”.

## 5. KUTHIBITI KWA MWEZI WA RAMADHANI NI KWA KUUONA MWEZI,

« لَا تَصُومُوا حَتَّى تَرَوْا الْهَيْلَالَ وَلَا تُفْطِرُوا حَتَّى تَرَوْهُ فَإِنْ غَمَّ عَلَيْكُمْ فَاقْدُرُوا لَهُ »

“Msifunge mpaka muuone mwezi mwandamo, na wala msifuturu mpaka muuone (mwezi mwandamo) mkizuliwa (na mawingu n.k) basi ukadirieni (kwa kukamilisha siku 30 za mwezi wa shabani)<sup>5</sup>”.

### • AU KUPEWA HABARI HABARI NA MTU MUADILIFU:

« تَرَأَى النَّاسُ الْهَيْلَالَ، فَأَخْبَرْتُ رَسُولَ اللَّهِ -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- أَنِّي رَأَيْتُهُ فَصَامَ وَأَمَرَ

النَّاسَ بِصِيَامِهِ »

“Watu walionyeshana mwezi mwandamo, nikamueleza Mtume swala na salamu zimfikie kwamba mimi (Ibn Umar) nimeuona, akafunga na akaamrisha watu wengine kufunga<sup>6</sup>”

## 6. UBORA NA UTUKUFU WA MWEZI WA RAMADHANI:

« إِذَا جَاءَ رَمَضَانُ فَتَبَحَّتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، وَغُلِقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ، وَصُفِّدَتِ الشَّيَاطِينُ »

“Inapoingia Ramadhani milango ya pepo inafunguliwa, na milango ya moto inafungwa, na mashetani wanafungiwa<sup>7</sup>”.

<sup>4</sup>- Bukhari (8) na Muslim (120).

<sup>5</sup>- Bukhari (1906) na Muslim (2554).

<sup>6</sup>- Sunan Abi Daud (2342).

<sup>7</sup>- Muslim (1079).

«إِذَا كَانَ أَوَّلُ لَيْلَةٍ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ صُفِّدَتِ الشَّيَاطِينُ، وَمَرَدَةُ الْجِنِّ، وَغُلِقَتِ أَبْوَابُ النَّارِ، فَلَمْ يُفْتَحْ مِنْهَا بَابٌ، وَفُتِّحَتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، فَلَمْ يُغْلَقْ مِنْهَا بَابٌ، وَيُنَادِي مُنَادٍ: يَا بَاغِيَ الْخَيْرِ أَقْبِلْ، وَيَا بَاغِيَ الشَّرِّ أَقْصِرْ، وَلِلَّهِ عُتَقَاءُ مِنَ النَّارِ، وَذَلِكَ كُلُّ لَيْلَةٍ»

“Unapokuwa usiku wa mwanzo wa mwezi wa Ramadhani mashetani na wale majini waliobobea (kwa uasi) wanafungwa, na inafungwa milango ya moto wala haufunguliwi mlango wowote wa moto, na inafunguliwa milango ya pepo wala haufungwi mlango wowote wa pepo, na atasema msemaji: Ewe mwenye kutaka kheri sogea, na ewe mwenye kutaka shari jizuie, na ana Allaah watu anaowaacha huru na moto na hilo ni kila usiku<sup>8</sup>”.

## **7. FADHILA ZA KULA DAKU:**

« تَسَحَّرُوا فَإِنَّ فِي السَّحُورِ بَرَكَهً »

“Kuleni daku kwa sababu katika daku kuna baraka<sup>9</sup>”.

- “Hakika Allaah na Malaika wake wanawaswali wenye kula daku<sup>10</sup>”.

## **8. BORA YA DAKU NI TENDE:**

« نِعْمَ سَحُورُ الْمُؤْمِنِ التَّمْرُ »

“Bora ya daku ya muislamu ni Tende”.

- Muislamu fahamu kwamba Daku ni miongoni mwa tafauti baina ya saumu yetu na saumu ya Mayahudi na Wakristo.

---

<sup>8</sup>- Sunan Tirmidh (682).

<sup>9</sup>- Bukhari (1923) na Muslim (1095).

<sup>10</sup>- Sahihi Ttarghiib (1066).

## 9. RUHUSA YA KUNYWA MAJI N.K BAADA YA ADHANA YA PILI:

«إِذَا سَمِعَ أَحَدُكُمْ النِّدَاءَ وَالْإِنَاءَ عَلَى يَدِهِ، فَلَا يَضَعُهُ حَتَّى يَقْضِيَ حَاجَتَهُ مِنْهُ»

“Atakaposikia mmoja wenu adhana (ya pili) na hali ya kuwa chombo (cha maji n.k) kipo mkononi mwake, asikiweke chini mpaka akamilishe haja yake ndani ya (chombo) hicho<sup>11</sup>”.

## 10. MUDA WA DAKU YA MTUME swala na salamu zimfikie:

«تَسَحَّرْنَا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، ثُمَّ قَامَ إِلَى الصَّلَاةِ»، قُلْتُ: كَمْ كَانَ بَيْنَ الْأَذَانِ وَالسَّحُورِ؟ " قَالَ: «قَدْرُ خَمْسِينَ آيَةً»

Amesema Zaid Bin Thabit (Allaah amridhie): “Tulikula daku pamoja na Mtume swala na salamu zimfikie, kisha akaondoka kwenda kuswali”, (Anas Bin Malik anasema:) nikauliza: ulikuwa ni muda gani baina ya adhana (ya pili) na (kumaliza kula) daku? Akasema (zaid): “kiasi cha kusoma aya hamsini<sup>12</sup>”.

## 11. WAJIBU WA KULALA NA NIA KATIKA USIKU WA RAMADHANI:

«مَنْ لَمْ يُجْمِعِ الصِّيَامَ قَبْلَ الْفَجْرِ، فَلَا صِيَامَ لَهُ»

“Yule ambaye hakuazimia (hakunuwia) saumu kabla ya alfajri hana funga<sup>13</sup>”.

- Nia inakuwa moyoni wala haitamkwi na inatosha kwa muislamu kunuwia usiku wa kwanza kwamba atafunga ramadhani yote, lakini ikitokea ameacha kufunga kwa maradhi, safari n.k atapoanza tena kufunga atanuwia upya.

<sup>11</sup>- Sunan Abi Daud (2349).

<sup>12</sup>- Bukhari (1921).

<sup>13</sup>- Sunan Abi Daud (2454).

## 12. FUNGA YA MWENYE KUAMKA NA JANABA ASUBUHI YA RAMADHANI:

Amesimulia Aisha na Ummu Salama (Allaah awaridhie) kwamba Mtume swala na salamu zimfikie alikuwa:

«يُذْرِكُهُ الْفَجْرُ وَهُوَ جُنْبٌ مِنْ أَهْلِهِ، ثُمَّ يَغْتَسِلُ، وَيَصُومُ»

“Inampata yeye alfajiri na hali ya kuwa ana janaba kutokana na wakeze, kisha anaoga na anafunga<sup>14</sup>”.

- Baadhi ya watu hudhani kwamba ukiamka na janaba saumu haisihi, sahihi ni kwamba utaoga na utaendelea na saumu.

## 13. FUNGA YA RAMADHANI INAFUTA MADHAMBIBI YALIYOPITA:

«مَنْ صَامَ رَمَضَانَ، إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا، غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

“Mwenye kufunga Ramadhanani kwa Imani na kutaraji ujira (kwa Allaah) atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia<sup>15</sup>”.

## 14. FUNGA NI KINGA YA KUIINGIA MOTONI:

«الصِّيَامُ جُنَّةٌ، وَحِصْنٌ حَصِينٌ مِنَ النَّارِ»

“Saumu ni kinga, na ni ngome madhubuti (ya kukuzuia) na moto<sup>16</sup>”.

## 15. AMEPATA HASARA AMBAYE HAKUSAMEHEWA KTK MWEZI WA RAMADHANI

«رَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ دَخَلَ عَلَيْهِ رَمَضَانُ ثُمَّ انْسَلَخَ قَبْلَ أَنْ يُغْفَرَ لَهُ»

“Ampata hasara mtu ambaye imemuingilia yeye Ramadhanani kisha ikaondoka kabla hajasamehewa<sup>17</sup>”.

<sup>14</sup>- Bukhari (1926).

<sup>15</sup>- Bukhari (38) na Muslim (759).

<sup>16</sup>- Sahihil Jaamii (3880).

<sup>17</sup>- Sunan Tirmidh (3545).

## 16. MALIPO YA WAFUNGAJI SIKU YA KIAMA:

« إِنَّ فِي الْجَنَّةِ بَابًا يُقَالُ لَهُ الرَّيَّانُ، يَدْخُلُ مِنْهُ الصَّائِمُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، لَا يَدْخُلُ مِنْهُ أَحَدٌ غَيْرُهُمْ، يُقَالُ: أَيْنَ الصَّائِمُونَ؟ فَيَقُومُونَ لَا يَدْخُلُ مِنْهُ أَحَدٌ غَيْرُهُمْ، فَإِذَا دَخَلُوا أُغْلِقَ فَلَمْ يَدْخُلْ مِنْهُ أَحَدٌ»

“Hakika peponi kuna mlango unaitwa Rayyaan, wataingia kupitia mlango huo siku ya kiama wafungaji, hatoingia kupitia mlango huo mtu yayote asiyekuwa wao<sup>18</sup>”.

## 17. THAMANI YA HARUFU YA KINYWA CHA MFUNGAJI:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَخُلُوفٌ فَمِ الصَّائِمِ أَطْيَبُ عِنْدَ اللَّهِ تَعَالَى مِنْ رِيحِ الْمِسْكِ»

“Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mikononi mwake (wallaahi) harufu ya kinywa cha mfungaji inapendeza Zaidi mbele ya Allaah Ta’alaa kuliko harufu ya miski<sup>19</sup>”.

## 18. MIONGONI MWA UKAMILIFU WA FUNGA YA MTU NI KUACHA UPUUZI:

«إِنَّ الصِّيَامَ لَيْسَ مِنَ الْأَكْلِ وَالشُّرْبِ فَقَطْ، إِنَّمَا الصِّيَامُ مِنَ اللَّغْوِ وَالرَّفَثِ»

“Funga si kuacha kula na kunywa tu, hakika funga ni (kujiepusha) na pumbao na maneno machafu<sup>20</sup>”.

## 19. BAADHI YA ADABU MUHIMU KWA MFUNGAJI:

«وَإِذَا كَانَ يَوْمُ صَوْمِ أَحَدِكُمْ فَلَا يَرْفُثْ وَلَا يَصْخَبْ، فَإِنْ سَابَهُ أَحَدٌ أَوْ قَاتَلَهُ فَلْيَقُلْ إِنِّي امْرُؤٌ صَائِمٌ»

“Itakapokuwa siku ya funga ya mmoja wenu asiseme maneno machafu, wala asipige kelele, na mtu yeyote akimtukana au kutaka kupigana nae yeye aseme: mimi ni mtu niliyefunga<sup>21</sup>”.

<sup>18</sup>- Bukhari (1896) na Muslim (1152).

<sup>19</sup>- Bukhari (1894) na Muslim (1151).

<sup>20</sup>- Sahihi Bin Hibbaan (3479).

<sup>21</sup>- Bukhari (1904) na Muslim (1151).

## 20. HAITAKIWI KUBALIGHISHA MAJI (KUYAVUTA SANA) PUANI WAKATI WA KUTAWADHA:

Inafahamika kwamba ni sunna mtu anapotawadha kuingiza maji puani na kuyavuta kisha kuyapenga kwa mkono wa kushoto, lakini unapokuwa umefunga hautayavuta, tafauti na baadhi ya watu wanatia vidole puani badala ya maji na wengine hupenga kwa kutumia mkono wa kulia

«وَبَالِغٌ فِي الْأَسْتِنَاقِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ صَائِمًا»

“Na Balighisha wakati wa kupandisha (maji puani) isipokuwa uwe umefunga<sup>22</sup>”.

## 21. MTU ALIYEKULA MCHANA WA RAMADHANI KWA KUSAHAU:

«إِذَا نَسِيَ فَأَكَلَ وَشَرِبَ، فَلَيْتَمَّ صَوْمُهُ، فَإِنَّمَا أَطْعَمَهُ اللَّهُ وَسَقَاهُ»

“Akisahau akala au akanywa (bila kukusudia) basi akamilishe saumu yake, hakika Allaah ndiye amemlisha na kumnywesh<sup>23</sup>”.

## 22. IMEBATILIKA FUNGA YA MTU ALIYEJITAPISHA:

« مَنْ ذَرَعَهُ قِيءٌ وَهُوَ صَائِمٌ فَلَيْسَ عَلَيْهِ قِضَاءٌ وَإِنْ اسْتَقَاءَ فَلْيَقْضِ »

“Yule ambaye yamemshinda yeye (hakuweza kuyazuia) matapishi hali ya kuwa amefunga (akatapika) hakuna juu yake kulipa (funga hiyo), na akijitapisha (makusudi) basi alipe<sup>24</sup>”.

---

<sup>22</sup>- Sunan Abi Daud (142).

<sup>23</sup>- Bukhari (1933) na Muslim (1155).

<sup>24</sup>- Sunan Abi Daud (2382).

### **23. INAFAA KUJIMWAGIA MAJI BARIDI KICHWANI KWA SABABU YA KIU AU JOTO KALI KATIKA MCHANA WA RAMADHANI:**

Amesimulia Swahaba kwamba:

«لقد رأيتُ رسولَ الله -صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- بِالْعَرَجِ يَصُبُّ عَلَى رَأْسِهِ الْمَاءَ وَهُوَ صَائِمٌ مِنَ الْعَطَشِ، أَوْ مِنَ الْحَرِّ»

“Hakika nilimuona Mtume swala na salamu zimfikie katika (sehemu inayoitwa ‘Arji) akimimina kichwani mwake maji hali ya kuwa amefunga kutokana na Kiu au Joto kali<sup>25</sup>”.

### **24. INAFAA KUMBUSU AU KUMKUMBATA MKEO KATIKA MCHANA WA RAMADHANI:**

Amesimulia Aisha (Allaah amridhie) kwamba Mtume swala na salamu zimfikie alikuwa:

«يُقْبَلُ وَيُبَاشِرُ وَهُوَ صَائِمٌ، وَكَانَ أَمْلَكُكُمْ لِإِزْبِهِ»

“Anabusu na kukumbatia hali ya kuwa amefunga, na alikuwa anamiliki zaidi matamanio yake (kuliko nyinyi)<sup>26</sup>”.

- Tahadhari kwa vijana na jambo hili bora uache.

### **25. MALIPO YA KUMFUTURISHA MFUNGAJI:**

«مَنْ فَطَرَ صَائِمًا كَانَ لَهُ مِثْلُ أَجْرِهِ، غَيْرَ أَنَّهُ لَا يَنْقُصُ مِنْ أَجْرِ الصَّائِمِ شَيْئًا»

“Atakaemfuturisha mfungaji (yeyote) atapata mfano wa malipo yake (huyo aliye mfuturisha), na wala hapunguzi katika malipo ya mfungaji (huyo) kitu chochote<sup>27</sup>”.

<sup>25</sup>- Sunan Abi Daud (2365).

<sup>26</sup>- Bukhari (1927) na Muslim (1106).

<sup>27</sup>- Sunan Abi Daud (807).

## 26. FURAHA YA MFUNGAJI DUNIANI NA AKHERA:

«لِلصَّائِمِ فَرْحَتَانِ: فَرْحَةٌ عِنْدَ فِطْرِهِ، وَفَرْحَةٌ عِنْدَ لِقَاءِ رَبِّهِ»

“Ana mfungaji furaha mbili: Furaha wakati wa kufuturu kwake, na Furaha wakati atapokutana na Mola wake Mlezi<sup>28</sup>”.

## 27. SUNNA NI KUANZA KUFUTURU KWA TENDE:

يُفْطِرُ عَلَى رُطَبَاتٍ قَبْلَ أَنْ يُصَلِّيَ فَإِنْ لَمْ تَكُنْ رُطَبَاتٍ فَعَلَى تَمْرَاتٍ فَإِنْ لَمْ تَكُنْ حَسَا حَسَوَاتٍ مِنْ مَاءٍ.

Mtume alikuwa “anafuturu kwa tende (mbichi) kabla ya kuswali (maghrib), akikosa basi tende kavu, na akikosa achota fumba la maji<sup>29</sup>”.

## 28. KUHARAKISHA KUFUTURU NI SUNNA NA NDIO KHERI:

«لَا يَزَالُ النَّاسُ بِخَيْرٍ مَا عَجَّلُوا الْفِطْرَ»

“Watu hawataacha kuwa katika kheri muda wa kuwa wanaharakisha kufuturu<sup>30</sup>”.

## 29. MUDA WA KUFUTURU:

«إِذَا أَقْبَلَ اللَّيْلُ مِنْ هَا هُنَا، وَأَدْبَرَ النَّهَارُ مِنْ هَا هُنَا، وَغَرَبَتِ الشَّمْسُ فَقَدْ أَفْطَرَ الصَّائِمُ»

“Ukija usiku kutokea upande huu (mashariki), na ukaondoka mchana upande huu (magharibi) na likazama jua hapo amefuturu mfungaji<sup>31</sup>”.

---

<sup>28</sup>- Muslim (1151).

<sup>29</sup>- Sunan Abi Daud (2358).

<sup>30</sup>- Bukhari (1957) na Muslim (1098).

<sup>31</sup>- Bukhari (1954) na Muslim (1100).

### 30. DUA BAADA YA KUFUTURU:

«ذَهَبَ الظَّمُّ وَأَبْتَلَّتِ العُرُوقُ وَثَبَّتِ الأَجْرُ إِنِ شَاءَ اللهُ»

“Kimeondoka kui, imerowa (imelainika) mishipa na yatathibiti malipo In Shaa Allaah<sup>32</sup>”.

### 31. KISIMAMO CHA RAMADHANI / SWALA YA TARAWEIH:

«مَنْ قَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا، غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

“Mwenye kuswali katika mwezi wa Ramadhani (taraweih) kwa Imani na kutarajia malipo, atasamehewa madhambi yake yaliyopita<sup>33</sup>”.

Namuomba Allaah aitakabali amali yangu hii na aweke taufiq kama ninavyomuomba atukubalie Swala, Funga na Ibada zetu mbalimbali katika mwezi wa Ramadhani na miezi mingine na atuhifadhi sisi na ndugu zetu waislamu Duniani na janga hili la Covid (19) na awape shifaa wale waliosibiwa na amlipe ujira wa shahidi yule aliyekufa kwa sababu hiyo.

Swala na salamu zimfikie tume wetu Muhammad, Jamaa zake  
na Maswahaba pia.

**ABU HALIMA ARAFAT BIN MAHMOUD**

**PONGWE-TANGA**

**TANZANIA**

**AL-KHAMIS 30/SHA'BANI/1441H – 23/4/2020M.**

---

<sup>32</sup>- Sunan Abi Daud (2357).

<sup>33</sup>- Bukhari (37) na Muslim (759).